# Iyelele Amefufuka

Comp: Wachira Sammy
*St Gregory Choir. Vol 2*
+254720883008




Copyright © <February 2016- Malindi Kenya samirmuriuki@gmail.com
All Rights Reserved







1. (a) Mbiu ya mgambo ikilia kuna jambo (jambo gani) tegeni masikio yenu niwaarifu
   (b) Leo asubuhi na mapema ametoka (kaburini) tumshangilie Mwokozi amefufuka.

***Yu hai Mwokozi Yesu amefufuka, kaburini ametoka leo yu hai.***
***Dunia ishangilie na kufurahi aleluya ukombozi umetimia, tumshangilie***
***(Iyelele yelele yelele iyelele njoni tuimbe, iyelele yelele yelele iyelele Amefufuka)x2***

2. (a) Wayahudi walifikiria wameshinda (bali kumbe) walikuwa wamesahau alishasema
   (b) Atakufa na kufufuka siku ya tatu (wayahudi) waliaibika na kusema ameibiwa.

3. (a) Mungu kaupenda ulimwengu hata sasa (kamtoa) mwanaye wa pekee afe msalabani
   (b) ili wokovu na huruma yake Mungu (Mungu wetu) zitufikie sisi watoto wake.

4. (a) Yesu aliteswa kwa 'jili ya dhambi zetu (wanadamu) huu ni upendo wa pekee na wa ajabu
   (b) nasi tuwapende pia na ndugu zetu (na jirani) nasi tuuone upendo wa Mungu wetu.